**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

---

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

***Dodoma*** ***Mei, 2020***

# YALIYOMO

**1.0 UTANGULIZI....................................................1**

**2.0 MAJUKUMU YA WIZARA...........................................7**

**3.0 HALI YA SEKTA YA ARDHI NCHINI ............................9**

**4.0 MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI NCHINI .................12**

**5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2020/21 ...............................................15**

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48** ........................................ 15

**Mapato** ........................................................................................ 15

**Matumizi** ..................................................................................... 18

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03** ...................................... 19

**Mapato** ........................................................................................ 19

**Matumizi** ............................................. **Error! Bookmark not defined.**

**5.1 UTAWALA WA ARDHI .................................................21**

**Usimamizi wa sekta ya ardhi** ........................................................ 21

**Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria** ......................... 22

**Usimamizi wa Masharti ya Umiliki** .................................................. 25

**Uthamini wa Mali** ......................................................................... 26

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini** ............................................. 29

***Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*** .................................... 32

**Usimamizi wa Visiwa na Fukwe Nchini** ........................................... 33

**Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi** .................................................. 34

Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi ..... 34

**5.2 HUDUMA ZA TEHAMA ..... 36**

Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi ..... 36

**5.3 UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI ..... 38**

Utayarishaji wa Ramani za Msingi ..... 39

Upimaji wa ardhi nchi kavu ..... 41

Upimaji wa Viwanja na Mashamba ..... 41

Upimaji wa Mipaka ya Maeneo ya Hifadhi ..... 42

Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa ..... 43

Upimaji ndani ya maji ..... 45

**5.4 UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI ..... 45**

Upangaji na Usanifu wa Miji ..... 46

Utangazaji wa maeneo ya upangaji miji ..... 46

Uandaaji wa Mipango Kabambe ..... 47

Uandaaji wa Mipangokina ..... 48

Urasimishaji Makazi ..... 49

Uendelezaji miji ..... 50

Usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba ..... 51

Mikopo ya ujenzi wa nyumba ..... 52

Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali ..... 53

Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi ..... 55

**5.5 MIRADI YA MAENDELEO ..... 56**

**Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi** .......... 57

**Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi**.......... 58

**Mradi wa Upimaji Mipaka ya Kimataifa** .......... 60

**Mradi wa Kuwezesha Ushindani wa Sekta Binafsi (Sekta ya Ardhi)** . 61

**Ushiriki wa Wizara katika Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa**.......... 62

**Miradi mipya ya Wizara**.......... 66

**5.6 USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA........67**

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** .......... 67

**Shirika la Nyumba la Taifa** .......... 71

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi** .......... 79

**Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro**.......... 80

**5.7 UTAWALA NA RASILIMALI WATU ..........83**

**Utawala Bora na Uwajibikaji** .......... 84

**Mafunzo kwa Watumishi**.......... 86

**Habari na Elimu kwa Umma** .......... 86

**6.0 SHUKRANI ..........87**

**7.0 HITIMISHO ..........90**

**8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21 ..........91**

**Makadirio ya Mapato** .......... 91

**Makadirio ya Matumizi**.......... 91

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi** .......... 92

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** .......... 92

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika*;** naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**2.** ***Mheshimiwa Spika*;** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima, afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge la Bajeti. Aidha, kufuatia kifo cha Mhe. Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini,

kilichotokea mwezi Januari, 2020, Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Lwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kilichotokea mwezi Aprili, 2020, Mhe.Richard Mganga Ndassa aliyekuwa mbunge wa Sumve kilichotokea mwezi Aprili 2020 na Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga aliyekuwa mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria kilichotokea tarehe 1 Mei, 2020, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutoa pole kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, natoa pole kwa wananchi wote walioathiriwa kwa namna moja ama nyingine na majanga yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini hususan mafuriko na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi aina ya Corona (COVID-19). Tunawaombea marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi, Amina.

**3.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa namna ya kipekee, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kuendelea kutambua na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa uongozi makini katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa na kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

**4.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Serikali ya Awamu ya Tano tumeshuhudia mageuzi makubwa ndani ya sekta ya ardhi na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*standard gauge*); kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi wa bwawa la uzalishaji umeme la Julius Nyerere na Ujenzi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambayo inatarajiwa kuleta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii kwa watanzania. Hakika uongozi wake mahiri umeendelea kuijengea heshima kubwa nchi yetu kitaifa na kimataifa.

**5.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa nyakati tofauti tumeshuhudia baadhi ya viongozi au wawakilishi kutoka nchi mbalimbali duniani wakitembelea Tanzania kujifunza kuhusu yanayoendelea katika nyanja za siasa, utawala, uwekezaji, mapambano dhidi

ya rushwa, nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi, mfumo wa utoaji elimu bila ada ngazi ya msingi hadi sekondari pamoja na masuala ya ukuzaji demokrasia na udumishaji wa amani nchini.

6. ***Mheshimiwa Spika;*** nawapongeza pia Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali wakilenga kuboresha huduma za msingi kwa Umma kama kichocheo cha kudumisha amani, upendo, mshikamano na utulivu nchini. Napenda kuwashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, nawapongeza Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd (Mb.), Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi imara katika kusimamia maslahi, ustawi wa wananchi wa Tanzania

Zanzibar na kuendelea kudumisha misingi ya Muungano wetu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge letu. Vilevile ninawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Tunawaombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuwapongeza Mhe. George Simbachawene Mbunge wa Kibakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Iddi Azzan Zungu Mbunge wa Ilala kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira na Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nawatakia kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

**9.** ***Mheshimiwa Spika;*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/20 na mwelekeo wa shughuli za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo na maagizo yanayoihusu Sekta ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali yanatimizwa ipasavyo.

**10.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mhe. Kemilembe Rose Julius Lwota (Mb.), kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia kwa kipindi chote pamoja na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48** –

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03 –** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, ninawashukuru kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na kutoa mwelekeo mpya wa mabadiliko katika Sekta ya Ardhi.

**11.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ismani kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kujiletea maendeleo yao binafsi pamoja na Taifa kwa ujumla.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

**12.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo: -

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;
ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;
iii) Kusimamia utawala wa ardhi;
iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;
v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;
vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hati za hakimiliki ya kimila;
vii) Kusajili hatimiliki za ardhi, nyaraka za kisheria na kuimarisha usalama wa milki;
viii) Kusimamia uthamini wa mali nchini;
ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;
x) Kusimamia uendelezaji milki;
xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi;
xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;

xiv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro; na,

xv) Kusimamia maslahi, utendaji kazi na maendeleo ya watumishi wa Wizara.

## 3.0 HALI YA SEKTA YA ARDHI NCHINI

**13.** ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Ardhi imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa kila mwananchi na Taifa kwa ujumla hasa kwa kuwa mhimili na kichocheo cha uwekezaji na uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini, miundombinu na hivyo kuongeza ajira na kukuza pato la Taifa.

**14.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuhakikisha Sekta ya Ardhi inaimarika zaidi, Wizara imeendelea kujenga mifumo ya utawala na usimamizi wa ardhi kwa kuanzisha Ofisi za ardhi za Mikoa yote **26** pamoja na kuendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi ngazi ya Halmashauri zote nchini

**15.** ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara imeendelea kufanya mageuzi katika utumiaji wa teknolojia katika utoaji wa huduma za ardhi. Hali hii imerahisisha mifumo ya upangaji, upimaji, usimamizi wa ardhi, usajili na utoaji hati, na uhifadhi wa kumbukumbu. Utumiaji wa teknolojia pia umeongeza uwazi katika utendaji kazi na upatikanaji wa taarifa hivyo kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migogoro.

**16.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyokuwa imekithiri nchini. Aidha, katika utatuzi wa migogoro ya ardhi, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya msingi yanayohusu Sekta ya Ardhi.

**17.** ***Mheshimiwa Spika;*** hali ya uendelezaji wa makazi nchini imeendelea kuimarika kwa kutekeleza programu na mikakati ya upangaji na urasimishaji makazi nchini. Wizara imeendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji, sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika kutekeleza kazi hizo. Vilevile, Wizara

imeendelea kuandaa na kusimamia miongozo mbalimbali ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

**18.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuimarisha huduma za upimaji wa ardhi nchini kwa kusimika miundombinu ya mtandao mpya wenye alama za upimaji **831** nchi nzima zinazorahisisha upimaji wa ardhi ndani ya kilometa **40**. Pamoja na juhudi hizi, Serikali inaendelea kuongeza alama hizo ili kupunguza umbali kati ya alama moja na nyingine utakaosaidia kupunguza gharama za upimaji.

**19.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuimarisha usalama wa milki kwa wananchi kwa kurahisisha mifumo ya utoaji hati, utambuzi wa vipande vya ardhi mijini na vijijini na upatikanaji wa taarifa za wamiliki. Vilevile, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya sera, sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi.

## 4.0 MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI NCHINI

**20.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 hadi 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati wa kuzindua Bunge la 11 mwezi Novemba, 2015; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013-2033); Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000; pamoja na sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

**21.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kuzingatia nyaraka na miongozo hiyo muhimu, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kwa makini masuala yaliyomo yanayohusu Sekta ya Ardhi mwaka hadi mwaka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa na Serikali. Mwelekeo wa Wizara ni kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma karibu na maeneo ya wananchi ili kuwa na uhakika wa

milki salama, nyumba bora, makazi endelevu, mifumo imara ya upimaji ardhi, ukusanyaji wa maduhuli na kumbukumbu za ardhi nchini.

**22.** ***Mheshimiwa Spika;*** ardhi ni rasilimali muhimu kwa jamii na matumizi yake ni mtambuka hivyo maendeleo katika sekta mbalimbali nchini yanategemea ardhi. Wizara itaendelea kuhakikisha ardhi inatumika kwa ajili ya kuongeza uwekezaji katika uzalishaji mali, kilimo, viwanda, ufugaji, uchimbaji madini, ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ambayo itaongeza ajira, mapato na mauzo ya nje. Serikali itaendelea kutambua na kuhakiki uwekezaji katika ardhi ili kutambua mchango wake katika uchumi wa nchi.

**23.** ***Mheshimiwa Spika;*** migogoro ya ardhi kwa muda mrefu imekuwa ni kero kwa wananchi nchini. Katika kuhakikisha migogoro hiyo inakoma Wizara imekuwa ikishirikiana na Wizara nyingine za kisekta na taasisi mbalimbali kuhakikisha migogoro hiyo inatatuliwa na kupunguza uwezekano wa kuibuka kwa migogoro mipya. Wizara itaendelea kujenga uelewa kwa wananchi na wadau kuhusu masuala mbalimbali ya

ardhi pamoja na kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa jamii. Vilevile, Wizara itaendelea kujenga Mifumo ya Kitaasisi itakayosaidia utatuzi wa migogoro.

**24.** ***Mheshimiwa Spika;*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na hali ya Sekta ya Ardhi, naomba sasa nitoe ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**), pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka wa fedha 2019/20 na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2020/21. Takwimu za utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 30 Aprili, 2020. Hotuba hii inatoa pia taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2015/16 hadi 2019/20).

## 5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2020/21

**25.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Fungu **48**-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48**

***Mapato***

**26.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **180** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imekusanya shilingi bilioni **84.5** sawa na asilimia **47** ya lengo (**Jedwali Na. 1A & Na. 1B).**

**27.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kipindi cha miaka mitano, hali ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi imeendelea kuimarika. Makusanyo haya yameongezeka kutoka shilingi **bilioni 74.71** mwaka

2015/16 hadi kufikia wastani wa shilingi **bilioni 100** mwaka 2019/20 **(Jedwali Na.2).** Ongezeko hili limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na Wizara ikiwemo kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki na kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi. Wizara inaendelea kuweka utaratibu wa namna ya kuhakikisha kila mmiliki wa ardhi anachangia pato la Taifa kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na sekta ya ardhi.

**28.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kuhamasisha na kufuatilia wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari. Natumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. **Natoa rai kwa wananchi waliopimiwa ardhi, kutambuliwa milki zao na kumilikishwa kulipa kodi kwa wakati ili kuepuka tozo ya adhabu au hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao.**

**29.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu inatarajia kukusanya shilingi **bilioni 200** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri itakayosaidia ukusanyaji wa mapato kwa urahisi;

ii) Kuboresha kanzidata ya wamiliki wa ardhi kwa kutumia mfumo unganishi wa kielektroniki utakaosaidia kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na kuwasiliana na wamiliki kwa urahisi kupitia mawasiliano ya simu na barua pepe;

iii) Kushirikiana na Serikali za Mitaa kusambaza hati za madai, kufuatilia malipo ya madeni na kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

iv) Kuongeza wigo wa makusanyo kwa kuwahamasisha wananchi kumilikishwa viwanja vilivyopimwa pamoja na kutambua

na kusajili wamiliki wa kila kipande cha ardhi katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa;

v) Kupima maeneo ya uchimbaji wa madini na kutoza kodi stahiki;

vi) Kuhakiki matumizi ya ardhi iliyomilikishwa yakiwemo maeneo ya taasisi za umma na za kidini ili sehemu ya ardhi inayotumiwa kibiashara itozwe kodi stahiki;

vii) Kuweka utaratibu wa kutoza kodi ya pango la ardhi kwa mashamba makubwa yanayotumika kibiashara;

viii) Kutambua na kutoza kodi wamiliki wenye Hatimiliki za Sehemu ya Jengo (Unit Titles); na

ix) Kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

**Matumizi**

**30.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliidhinishiwa shilingi **bilioni 63.9** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya

maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 17.4** zilikuwa kwa ajili ya mishahara; shilingi **bilioni 19.7** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **bilioni 26.8** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya Shilingi **bilioni 6.48** kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni na Watumishi baada ya uhakiki uliofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango na kuifanya bajeti kuwa jumla ya shilingi bilioni **63.9.** Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara ilipokea shilingi **bilioni 40.5** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **63.4** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **14.9** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **bilioni 15.8** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi **bilioni 9.8** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 3)**.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03**

***Mapato***

**31.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitarajia kupata **shilingi milioni 706.** Kati ya fedha hizo, shilingi **milioni 700** ni kutoka kwa wadau

wa kimkakati na shilingi **milioni 6** ni kutokana na makusanyo ya kodi ya pango la nyumba za Tabora. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Tume imepokea shilingi milioni **446.58** sawa na asilimia **63.3** ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **435.61** ni fedha kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni **10.97** ni mapato ya ndani.

***Matumizi***

**32.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume iliidhinishiwa shilingi **bilioni 5.24** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 1.27** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi **milioni 979.82** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **bilioni 3.00** ni kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Tume ilipokea kiasi cha shilingi bilioni **1.53** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **29.1.** Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **922.06** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni **604.85** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## 5.1 UTAWALA WA ARDHI

***Usimamizi wa sekta ya ardhi***

**33.** ***Mheshimiwa Spika;*** utawala wa ardhi unalenga kuhakikisha ardhi yote nchini inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kwa lengo la kuboresha huduma katika uwekezaji, uboreshaji wa makazi, milki salama na kuwa kichocheo cha kuinua uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla. Majukumu haya yanatekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza sekta ya ardhi.

**34.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa huduma za sekta ya ardhi zinapatikana karibu na wananchi ili kuwapunguzia usumbufu na gharama za upatikanaji wake. Juhudi za kusogeza huduma hizi kwa wananchi zilianza kwa kuanzisha Ofisi za Ardhi katika Kanda tisa (**9**). Pamoja na juhudi hizo, bado wananchi wamekuwa wakipata usumbufu na kutumia gharama kubwa kuzifikia Ofisi hizo. Kwa muktadha huu, Wizara imeanzisha Ofisi za Ardhi katika Mikoa yote **26** nchini ambapo huduma zote za upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na

Nyaraka, ramani na michoro zitapatikana katika ofisi hizo. **Natoa rai kwa wananchi na viongozi wa Mikoa na Halmashauri kutoa ushirikiano na kuzitumia ofisi hizo kupata huduma za ardhi.**

**35.** ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara yangu imeendelea kuziimarisha Ofisi za Ardhi katika Halmashauri zote nchini kwa kuwapanga na kuwasimamia watumishi wa sekta ya ardhi wa kada zote kwa uwiano sawia. Aidha, Wizara itaendelea kuzipatia ofisi hizo vitendea kazi, rasilimali fedha pamoja na watumishi wa kada zinazohitajika ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma.

***Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria***

**36.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu uandaaji, usajili na utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, Hati za Hakimiliki za Kimila na Hatimiliki za Ardhi. Azma hii inalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi.

**37.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha miaka mitano,

Wizara imeratibu upimaji, uandaaji na usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **2,905** na hivyo kuzipatia Halmashauri za Vijiji mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kuandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **540** viliandaliwa. Hii inaifanya nchi kuwa na jumla ya vijiji **11,743** vilivyopimwa na kupewa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,319** vilivyopo nchini.

**38.** ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile, kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **375,259** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **150,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Jumla ya Hati za Hakimiliki ya Kimila **92,585** zimetolewa (**Jedwali Na. 4**). Kwa kipindi hicho jumla ya hati **1,516** zimetumika kama rehani ya mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 61.3** kwenye

taasisi za fedha.

**39.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imeratibu uandaaji na utoaji wa Hatimiliki **195,170** (**Jedwali:- 5A**), Nyaraka za Kisheria **255,662** (**Jedwali:- 5B**) na hati za umiliki wa sehemu ya jengo zipatazo **3,522** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuandaa na kutoa hatimiliki **100,000,** Nyaraka za Kisheria **50,000** na hati za umiliki wa sehemu ya jengo zipatazo **2,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya hatimiliki **37,870**, Nyaraka za Kisheria **55,179** na hati za umiliki wa Sehemu ya Jengo zipatazo **310** zimetolewa. Aidha, Wizara imesajili rehani za ardhi **3,070** chini ya Sheria ya Ardhi (Sura 113). Rehani hizo zimesaidia wananchi kupata mikopo na hivyo kuwanufaisha kiuchumi. **Natoa rai kwa wananchi waone umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria na kutumia nyaraka za umiliki walizopewa kuwainua kiuchumi.**

**40.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inakusudia kusajili na kutoa Vyeti

vya Ardhi ya Kijiji **100**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **520,000**, Hatimiliki **200,000**, nyaraka za kisheria **100,000**, hati za umiliki wa sehemu ya jengo **1,000** na rehani za ardhi kadri maombi yatakavyopokelewa na kusajiliwa. **Natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ili kuongeza usalama wa milki.**

***Usimamizi wa Masharti ya Umiliki***

**41.** ***Mheshimiwa Spika;*** Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki kuiendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilikagua mashamba **1,985** ili kujiridhisha uendelezaji wake. Kati ya hayo mashamba **45** yenye jumla ya ekari **121,032.2** umiliki wake ulibatilishwa baada ya kukiuka masharti ya Umiliki. Kati ya ekari hizo zilizobatilishwa ekari **12,448.5** zilitengwa kwa ajili ya uwekezaji na sehemu kuandaliwa mipango ya matumizi mengine na kugawiwa kwa wananchi kupitia mamlaka za upangaji. **Natoa wito kwa wamiliki wa mashamba kuyaendeleza kwa mujibu wa masharti ya umiliki. Serikali itachukua hatua**

**stahiki kwa wamiliki wote watakaokiuka masharti ikiwemo kufutiwa milki zao.**

**42.** ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kufanya utambuzi na ukaguzi wa mashamba ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Aidha, ardhi ya mashamba ambayo milki zake zitabatilishwa itakuwa sehemu ya hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kuwapatia wananchi wenye mahitaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji baada ya kupangwa na kupimwa upya.

***Uthamini wa Mali***

**43.** ***Mheshimiwa Spika;*** uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, na uidhinishaji wa taarifa za uthamini ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara yangu. Uthamini hufanyika ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, mizania,

kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

**44.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu iliidhinisha taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **52,645** na uthamini wa fidia wa mali **84,223** (**Jedwali Na. 6**). Katika kipindi hicho, Wizara pia imeshiriki kufanya uthamini wa mali katika maeneo ya miradi mikubwa ya kitaifa na ya kimkakati. Katika miradi hiyo, majedwali matatu (**3**) ya fidia yenye jumla ya wafidiwa **9,881** na fidia ya mali kiasi cha shilingi bilioni **113.9** yaliandaliwa na kuidhinishwa **(Jedwali Na.7).**

**45.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini **29,000**, ambapo kati ya hizo uthamini wa kawaida ni **10,000** na uthamini wa fidia ni **19,000** na kushughulikia malalamiko **120** ya uthamini wa fidia. Vilevile, Wizara ilipanga kuimarisha kumbukumbu za uthamini ikiwemo kukamilisha uhuishaji wa viwango

vya bei ya soko la ardhi katika mikoa **26**.

**46.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **34,276** ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni **13,060** na uthamini wa fidia **21,216** (**Jedwali Na. 8**). Jumla ya malalamiko **25** ya uthamini wa fidia yalipokelewa na kushughulikiwa kati ya malalamiko **120** yaliyotarajiwa. Kupungua kwa malalamiko kunatokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi na ushirikishwaji uliofanywa na wataalam wakati wa uthamini Aidha, jedwali la thamani ya mimea ambalo limekuwa likitumika kuanzia mwaka 2012 limehuishwa hivyo kuwa na jedwali jipya la viwango vya thamani ya mimea vya mwaka 2020. Kazi ya kuhuisha viwango vya bei ya soko la ardhi katika mikoa **26** inaendelea.

**47.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara yangu itaratibu uandaaji wa taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **15,700** na uthamini wa fidia wa mali **24,300**. Kadhalika, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko **120** ya uthamini wa fidia,

kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote **26** nchini.

***Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini***

**48.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa nchini kadri inavyojitokeza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Migogoro hiyo ipo katika sura mbili ambazo ni migogoro ya mipaka ya kiutawala na migogoro inayotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi. Sheria za ardhi zimeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia migogoro ya ardhi na pale inaposhindikana migogoro hiyo hupelekwa katika ngazi ya mahakama kutatuliwa.

**49.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu imekuwa na mikakati mbalimbali ya kushughulikia utatuzi wa migogoro. Mikakati hiyo ni pamoja na kushirikiana na viongozi wa Serikali, kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro, kuanzisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za halmashauri nchini, na programu ya '**Funguka kwa Waziri'.** Kupitia mikakati

hiyo jumla ya migogoro **15,808** ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala katika halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 9**). Pia, jumla ya migogoro **131,603** ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. **Natoa rai kwa viongozi na watumishi kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na maadili ya utumishi wa umma na kuendelea kushirikiana na wananchi katika utatuzi wa migogoro na kuepuka kusababisha migogoro mipya**.

**50.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi hiki cha miaka mitano, Wizara iliimarisha utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo ni mtambuka kwa njia shirikishi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta za OR-TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Maji, Kilimo, Viwanda, Ulinzi na Mazingira. Kupitia utaratibu huo, taarifa mbalimbali zinazohusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya ufugaji, kilimo, misitu, hifadhi za wanyamapori, vyanzo vya maji, hifadhi za mazingira, ulinzi, mipaka ya kiutawala na fidia ya ardhi ziliainishwa kutoka kwa waheshimiwa wabunge, sekta na halmashauri mbalimbali na kuandaa mapendekezo

yenye ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

**51.** ***Mheshimiwa Spika;*** kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Kamati ya Mawaziri wa Kisekta ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Kufuatia mapendekezo ya Kamati, Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Septemba, 2019, liliridhia kuwa vijiji **920** kati ya vijiji **975** vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vijiji **55** vilivyobaki ili kutoa maamuzi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali inaendelea kuhakiki mipaka, kupanga na kupima ili kuzipa Serikali za vijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za vijiji hivyo.

**52.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kiutawala na kushughulikia mashauri **500** yaliyopo na yatakayofikishwa

mahakamani. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, hadi tarehe 30 Aprili, 2020 migogoro ya Matumizi ya ardhi **5,892** ilishughulikiwa kiutawala. Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Wizara imepanga kutatua migogoro **1,000** ya umilikaji ardhi kiutawala.

***Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya***

**53.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayofanya kazi ya kupokea, kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **28,615** yaliyokuwepo na yatakayofunguliwa. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 mashauri mapya **15,841** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **44,456**. Kati ya hayo, mashauri **19,360** yaliamuliwa.

**54.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza azma ya kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/21, Serikali inakusudia kuhamishia

shughuli za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika mhimili wa Mahakama.

***Usimamizi wa Visiwa na Fukwe Nchini***

**55.** ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta ilifanya uhakiki uwandani wa visiwa **289** nchini na kuandaa taarifa kuhusu namna bora ya kuvisimamia, kudhibiti na kuviendeleza. Visiwa hivyo vyenye ukubwa tofauti na matumizi mbalimbali vinasimamiwa na mamlaka zaidi ya moja. Mamlaka hizo zinajumuisha Hifadhi za Taifa (TANAPA), Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), Wizara ya Ulinzi, Wakala wa Misitu na Serikali za Mitaa.

**56.** ***Mheshimiwa Spika;*** tathmini iliyofanyika imebaini kuwepo kwa changamoto katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa na fukwe nchini. Hali hii imesababisha baadhi ya visiwa na fukwe kutumika kama maficho ya wahalifu, njia za kupitisha bidhaa za magendo, uhamiaji haramu, na pia kuna uharibifu mkubwa wa mazingira. Katika kukabiliana na changamoto hizo,

Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 itaimarisha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa na fukwe ili kuwa na matumizi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

***Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi***

**57.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara yangu kupitia Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi ina jukumu la kuidhinisha maombi ya umilikishaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji fukwe, pamoja na maeneo ya kimkakati yenye maslahi ya umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Kamati ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **527** ya umilikishaji ardhi. Kati ya hayo, maombi **331** yalikuwa ya uwekezaji na **196** ya viwanja vya fukwe, ofisi za Balozi na Mashirika ya Kimataifa (**Jedwali Na. 10**). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi kutimiza majukumu yake.

***Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi***

**58.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu inasimamia shughuli za bodi mbalimbali za Wataalam wa sekta ya ardhi. Bodi hizo ni; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Wathamini na Bodi ya Usajili wa

Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kutoa adhabu kwa ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma. Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya Wataalam wa Mipangomiji **158,** Wathamini **114** na Wapima Ardhi **134** walisajiliwa na bodi zao. Aidha, jumla ya kampuni za upangaji **57,** upimaji **22** na uthamini **42** zimesajiliwa na kufikia jumla ya kampuni za upangaji **76** na upimaji **82** (**Jedwali Na. 11A,11B na 11C**). Uwepo wa wataalam na kampuni hizo umesaidia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na urasimishaji ardhi.

**59.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuendelea kusimamia weledi na maadili ya utendaji kazi, Wizara kwa kushirikiana na bodi za wataalam wa sekta ya ardhi ilibaini ukiukwaji wa maadili unaofanywa na baadhi ya kampuni ikiwemo kuongeza gharama za upangaji na upimaji kinyume na miongozo iliyowekwa na Wizara. Kampuni za upangaji tano **(5)** na ya upimaji moja **(1)** zimefutiwa usajili na wataalam watano (**5**) wa mipangomiji na mpima ardhi mmoja **(1)** wamechukuliwa hatua za kinidhamu.

## 5.2 HUDUMA ZA TEHAMA

***Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi***

**60.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ilibuni na kutekeleza Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) na kujenga Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Huduma za ardhi kwa kutumia Mfumo wa ILMIS zinatolewa katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam. Mfumo huu umerahisisha utoaji wa huduma za ardhi ambapo muda wa utoaji hati umepungua kutoka siku **90** hadi siku saba (**7**) endapo mwombaji atawasilisha nyaraka zote zinazohitajika kwa wakati.

**61.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuendelea kuunganisha mfumo wa ILMIS na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara imekamilisha kuunganisha mfumo huo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Hati za kielektroniki zinatolewa. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kuboresha mfumo kwa

kujenga miundombinu, kuchambua, kupiga picha (scanning) na kuhifadhi michoro, ramani na hati katika Ofisi za ardhi za mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini.

**62.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu imeendelea kuwekeza, kuboresha na kuongeza kasi katika matumizi ya mifumo ya kidigitali ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika kutekeleza haya, Wizara imesimika Mfumo wa Ofisi Mtandao (***e-office)*** ambao unasaidia katika mawasiliano na kutoa maamuzi kwa wakati. Sambamba na hilo, Wizara ilinunua na kusambaza mashine za kieletroniki (*Point of Sales Machine-PoS*) **238** kwenye ofisi za ardhi zilizoko katika Halmashauri zote nchini na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mashine hizo zinarahisisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Wizara pia imeunganisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli ya sekta ya ardhi katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (*GePG*). Hivyo, kwa kutumia simu ya mkononi mwananchi anaweza kulipa kodi ya pango

la ardhi kupitia simu yake.

**63.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. Wizara imewezeshwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kuunganisha Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (NLIC) na Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet). Pia, imeunganisha mifumo ya kutunza kumbukumbu za ardhi na Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili kuhakiki uraia wa wamiliki wa ardhi nchini.

**64.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya ardhi wa kutumia Mifumo ya TEHAMA, Wizara iliendesha mafunzo ya matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA kwa watumishi **422** kutoka Halmashauri na Sekretarieti za mikoa yote nchini.

## 5.3 UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

**65.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za upimaji ardhi wa nchi kavu na ndani ya maji, na utayarishaji

wa ramani za msingi kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali. Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu hayo.

***Utayarishaji wa Ramani za Msingi***

**66.** ***Mheshimiwa Spika***; kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imepiga picha za anga na kuandaa ramani picha yenye uwiano mkubwa wa **1: 2,500** katika Mkoa wa Dar es Salaam na sehemu ya Mkoa wa Pwani kwa eneo la ukubwa wa kilometa za mraba **4,300**. Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara imehuisha ramani za msingi **144** za uwiano mdogo wa **1: 50,000** katika mikoa ya Dodoma, Geita, Songwe na Ruvuma. Ramani hizo zimewezesha kurahisisha upangaji na upimaji wa maeneo mbalimbali katika mikoa hiyo. Aidha, Wizara imehuisha ramani ya Tanzania na kuwa na ramani inayojumuisha mipaka ya Mikoa na Wilaya mpya, uoto wa asili, miundombinu ya usafirishaji, mito na maziwa (**Kiambatisho Na.1**)

**67.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana

na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeandaa ramani za uhakiki wa mali za wananchi waliopisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Morogoro hadi Makutopora Wilayani Manyoni yenye urefu wa kilometa **336.** Ramani hizi zilisaidia kuharakisha zoezi la uthamini wa mali na hivyo kuepusha migogoro ya malipo ya fidia (**Kiambatisho Na. 2).**

**68.** ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu iliahidi kuhuisha ramani za msingi **68** pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia 30 Aprili, 2020, ramani za msingi **68** zenye uwiano wa 1: 50,000 na ramani za Mikoa **23** zilihuishwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuhuisha ramani za msingi 66 katika wilaya mbalimbali nchini.

**69.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na OR - TAMISEMI imeendelea kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya maeneo ya utawala na hifadhi. Tafsiri hizo

zimewezesha kutatua migogoro ya mipaka kati ya Kijiji na kijiji, Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa pamoja na Vijiji na Hifadhi. Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya Matangazo ya Serikali (GN) **24** yalitafsiriwa kwa kupima na kuweka alama za mipaka ya utawala na hifadhi (**Jedwali Na. 12A, 12B, 12C & 12D**).

**Upimaji wa ardhi nchi kavu**

**70.** ***Mheshimiwa* Spika;** upimaji wa ardhi nchi kavu unajumuisha upimaji wa viwanja, mashamba, mipaka ya ndani ya nchi na mipaka ya kimataifa. Katika kuwezesha na kurahisisha upimaji kufanyika kwa ufanisi alama za msingi husimikwa ardhini. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imesimika alama za msingi za upimaji **191** za nyongeza katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga Kagera, Songwe na Ruvuma na kufanya kuwa na jumla ya alama za msingi **831** kutoka alama **640** za awali. Wizara itaendelea kusimika alama za msingi mpya **150** katika mwaka wa fedha 2020/21.

***Upimaji wa Viwanja na Mashamba***

**71.** ***Mheshimiwa* Spika**; Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba

unaofanywa na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi. Upimaji huu huwezesha wananchi na taasisi mbalimbali kupata hatimiliki za ardhi na kutatua migogoro ya ardhi. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **988,526** na mashamba **5,940** kutoka Halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 13**).

**72.** ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu iliahidi kupokea na kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba **200,000** pamoja na kutatua migogoro **50** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 30 Aprili, 2020, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **222,849** na mashamba **268** ziliidhinishwa. Aidha, migogoro ya mipaka ya vijiji, hifadhi na ya Wilaya ilitatuliwa wakati wa upimaji.

***Upimaji wa Mipaka ya Maeneo ya Hifadhi***

**73.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jukumu la uhakiki na upimaji wa mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imehakiki na

kupima maeneo manne (**4**) ya Hifadhi za Taifa za Saadani, Serengeti, Rumanyika na Burigi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuhakiki na kupima mipaka ya maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi.

***Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa***

**74. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara ina jukumu la kuimarisha alama za mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Tanzania inapakana na nchi **10** kwa mpaka wenye urefu wa kilomita **1,841** nchi kavu na kilometa **2,086** ndani ya maji. Nchi na urefu wa mipaka yake ni kama ifuatavyo:- Uganda (km. **149** nchi kavu na km. **246** ndani ya maji), Kenya (km. **758** nchi kavu na km. **59.71** ndani ya maji), Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (km. **554** ndani ya maji), Burundi (km. **446** nchi kavu na km. **22.85** ndani ya maji), Malawi (km. **146** nchi kavu na km. **248** ndani ya maji), Rwanda (km. **230** ndani ya maji), Msumbiji (km. **51** nchi kavu na km. **670** ndani ya maji), Zambia (km. **289** nchi kavu na km. **56** ndani ya maji). Mipaka baina ya Tanzania na nchi za Comoro (km. **289.81** ndani ya maji) na Shelisheli (km. **341.88** ndani ya maji) inasubiri

kuidhinishwa na Umoja wa Mataifa. Aidha, Tanzania iliwasilisha Umoja wa Mataifa maombi ya nyongeza ya eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **60,000** nje ya ukanda wa kiuchumi baharini. Upatikanaji wa eneo hilo utaongeza wigo na fursa za kiuchumi ikiwemo uchimbaji wa mafuta na gesi.

**75.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeimarisha mpaka wenye urefu wa kilomita **172** za nchi kavu kati ya Tanzania na Kenya. Kazi zilizofanyika kuimarisha mpaka huu ni kufanya vikao vya pamoja vya majadiliano, kujenga alama mpya za msingi zilizoharibika, kuweka alama za katikati, ukarabati wa alama zilizoharibika, kupima alama za mpaka, kufyeka mkuza wa mpaka, kupima alama za picha za anga, kutambua majina ya kijiografia ya maeneo, kuandika majina na kupaka rangi alama za mpaka na kuandaa rasimu ya mkataba wa makubaliano ya mpaka. Wizara yangu itaendelea kuimarisha mipaka baina ya Tanzania na nchi jirani kwa mwaka wa fedha 2020/21.

***Upimaji ndani ya maji***

**76.** ***Mheshimiwa Spika;*** upimaji ndani ya maji ni moja ya jukumu la Wizara yangu. Upimaji huu husaidia kuandaa ramani elekezi za njia za vyombo vya usafiri ndani ya maji, kuainisha mipaka ya kimataifa na ujenzi wa mitambo ya uzalishaji umeme, gesi na mafuta, ujenzi wa madaraja, utafiti, kutandaza mabomba, kuongeza vina vya maji, ulinzi na usalama na uhifadhi wa mazingira. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipima bandari tano (**5**) za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga, Pemba na Wete. Upimaji huu umesaidia kuandaa ramani elekezi za njia za vyombo vya usafirishaji ndani ya maji katika bandari. Jumla ya ramani nane (**8**) zinazoonesha vina vya maji, miamba, mawimbi, mito na milima ziliandaliwa. Wizara yangu itaendelea kupima bandari na maeneo mengine ya ndani ya maji katika mwaka wa fedha 2020/21.

## 5.4 UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

**77.** ***Mheshimiwa Spika;*** upangaji miji na uendelezaji makazi ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara yangu. Majukumu haya yanajumuisha uandaaji wa mipango ya jumla (mipango

kabambe), mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji na vijiji, urasimishaji makazi pamoja na usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba.

**Upangaji na Usanifu wa Miji**

***Utangazaji wa maeneo ya upangaji miji***

**78.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu ina jukumu la kutangaza maeneo ya vijiji yanayokua na kufikia sifa ya kupangwa na kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007. Vigezo vya kutangaza maeneo hayo ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi, huduma za kiuchumi ikiwemo soko na maduka yasiyopungua matano **(5)**. Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye mamlaka za upangaji. Maeneo hayo huandaliwa mipango ya jumla na mipangokina na mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali.

**79.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka

mitano, Wizara ilipokea, kuidhinisha na kutangaza maeneo **72** kutoka katika mamlaka za upangaji. Maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya vijiji na kuwa maeneo ya mipangomiji na yanaendelea kuandaliwa mipangokina (**Jedwali Na. 14**). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipango miji.

***Uandaaji wa Mipango Kabambe***

**80.** ***Mheshimiwa Spika;*** ukuaji na uendelezaji wa miji huongozwa na mipango kabambe inayoainisha matumizi mbalimbali ya ardhi katika miji nchini. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliratibu uandaaji na kuidhinisha mipango kabambe **24** katika miji saba **(7)** Manispaa **13** na majiji manne **(4)**. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha Mipango Kabambe **6** na kufuatilia utelekezaji wake katika kanda tatu (**3**). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mipango Kabambe **7** imeandaliwa na

kuidhinishwa katika miji **3** manispaa **2** na majiji **2**. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango kabambe umefanyika katika Jiji la Arusha na Mji wa Korogwe na kuonesha uandaaji wa mipangokina unazingatia mipango kabambe. Aidha, mpango kabambe wa Manispaa ya Kigamboni umehuishwa kwenye mpango kabambe wa jiji la Dar es salaam (**Jedwali Na. 15**).

**81.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuunga mkono dhana ya Tanzania ya viwanda jumla ya ekari **284,349.07** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika miji mbalimbali nchini iliyoandaliwa mipango kabambe (**Jedwali Na. 16)**. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. **Natoa rai kwa mamlaka za upangaji kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji wake na kudhibiti uendelezaji miji ili uendane na mipango kabambe**

***Uandaaji wa Mipangokina***

**82.** ***Mheshimiwa Spika;*** mipangokina (michoro ya mipangomiji) huandaliwa na mamlaka za upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo yenye matumizi mbalimbali ikiwemo ya uwekezaji. Kwa

kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **6,143** yenye jumla ya viwanja **1,456,548** kutoka katika mamlaka za upangaji nchini.

**83.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, michoro ya Mipangomiji **1,195** yenye jumla ya viwanja **348,918** ilipokelewa na kuidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu inatarajia kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

***Urasimishaji Makazi***

**84.** ***Mheshimiwa Spika;*** urasimishaji makazi nchini unahusisha kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha maeneo yaliyoendelezwa bila kupangwa. Lengo la urasimishaji ni kuhakikisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili huduma za kijamii na miundombinu kwa njia shirikishi. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara

ilidhinisha michoro ya Mipangomiji ya urasimishaji yenye viwanja **703,836** katika Halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 17A)**. Kati ya viwanja hivyo, makampuni binafsi yalipanga viwanja **419,240.** (**Jedwali Na. 17B).**

**85.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliahidi kuendelea na zoezi la urasimishaji katika halmashauri katika kanda zote tisa (**9)** ambapo takriban viwanja/makazi **600,000** vitatambuliwa na kurasimishwa. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliandaa michoro ya urasimishaji **334** yenye viwanja/makazi **148,000** katika halmashauri mbalimbali nchini. Katika Mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi zitakazotekelezwa na mamlaka za upangaji nchini.

***Uendelezaji miji***

**86.** ***Mheshimiwa Spika;*** udhibiti wa uendelezaji miji ni suala mtambuka linalotekelezwa kwa kushirikisha Wizara na mamlaka za upangaji. Kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na kukua kwa

teknolojia, miji hubadilika na kuhitaji uratibu katika uendelezaji wake yakiwemo mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Kwa muktadha huu, Wizara yangu, ina jukumu la kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka mamlaka za upangaji. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha maombi **1,005** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

**87.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka Kanda tisa (**9**). Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **285** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka mamlaka za upangaji. Wizara itaendelea kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika mwaka wa fedha 2020/21.

***Usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba***

**88.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa nyumba nchini. Uendelezaji wa nyumba hufanywa na watu binafsi, taasisi za umma au binafsi, Shirika la Nyumba la Taifa, Vyama vya Ushirika wa

Nyumba na mamlaka mbalimbali za Serikali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na:- upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ubunifu wa nyumba za gharama nafuu, utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa serikali.

***Mikopo ya ujenzi wa nyumba***

**89.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ambapo: i) Mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kutoka taasisi za fedha kiasi cha shilingi **bilioni 29.87** kilitolewa kwa wananchi **1,914** (**Jedwali Na. 18A**); ii) Benki za biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimeongezeka kutoka tatu (**3**) hadi **34** ambapo, mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi **bilioni 438.58** ilitolewa kwa wananchi **5,460 (Jedwali Na. 18B)**; iii) Kiwango cha riba ya mikopo ya ujenzi wa nyumba katika taasisi za fedha kimeshuka kutoka kati

ya asilimia **21-23** hadi kufikia kati ya asilimia **13-18**; na iv) Muda wa kurejesha mikopo midogo midogo umeongezwa kutoka miaka mitano (**5**) hadi **10**.

***Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali***

**90.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali iliahidi kuongeza kiwango cha juu cha mkopo kinachotolewa na Mfuko kutoka shilingi milioni **20** hadi kufikia shilingi milioni **40.** Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali imeridhia ongezeko la kiwango cha mkopo hadi shilingi **milioni 40** ili kukidhi ongezeko la gharama za ujenzi wa Nyumba. Mikopo yenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 2.13** imeidhinishwa kwa watumishi **121**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi **403,719,092** yalikusanywa.

**91.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za Nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **139** ambao

wamejenga jumla ya nyumba **26,421** zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba vinne (4) vimeongezeka katika kanzidata na kufikia vyama vilivyo hai **38** ambavyo vimejenga jumla ya nyumba **1,056** katika Mikoa ya Dar es Salaam (**818**), Dodoma (**77**), Iringa (**16**), Kagera (**56**), Musoma (**22**), Morogoro (**36**), Mwanza (**15**) na Shinyanga (**16**). Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara yangu itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika.

**92.** ***Mheshimiwa Spika;*** pamoja na Wizara kuwa na kanzidata ya nyumba za waendelezaji miliki wa mashirika na taasisi mbalimbali, Wizara inaandaa utaratibu wa kufanya sensa ya nyumba nchi nzima na kuunda kanzidata ya nyumba kwa kutumia Mifumo unganishi ya kielektroniki ambayo inaweza kutumiwa na wadau wote wa sekta ya nyumba. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imefanya sensa ya majaribio

katika Wilaya ya Kondoa ikiwa ni hatua ya awali ya uboreshaji wa kanzidata.

### ***Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi***

**93.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa yenye lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji makazi. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imeshiriki katika mikutano **15** ya kimataifa. Mikutano hiyo iliwezesha kubuni uanzishwaji wa mfuko wa nyumba, ushiriki wa nchi katika kuandaa agenda za kimataifa za uendelezaji miji, upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu ya ujenzi wa nyumba kwa Shirika la Nyumba la Taifa, *Tanzania Investment Bank*, *Tanzania Mortgage Refinancing Company, AGM Holding Limited* na *Dar Village.*

**94.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/20, Wizara yangu iliahidi kusimamia na kuratibu ushirikiano wa Taasisi mbalimbali katika uendelezaji wa makazi nchini. Wizara yangu imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa

ambapo Tanzania iliweza kushiriki katika mikutano mitatu ya Kimataifa ikiwemo Mkutano wa kupitia mkataba wa masuala ya maliasili katika nchi za Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Nairobi Desemba, 2019, Kusanyiko la Wataalam wa Masuala ya Maendeleo ya Miji kwa kushirikiana na UN - Habitat lililofanyika Jijini Dodoma mwezi Januari, 2020, na Mkutano wa Kumi wa Jukwaa la Miji Duniani uliofanyika Abu Dhabi, Falme za Kiarabu mwezi Februari, 2020. Katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na Taasisi mbalimbali za Kimataifa kwa lengo la kutekeleza Malengo na mikakati inayoandaliwa na taasisi hizo.

### 5.5 MIRADI YA MAENDELEO

**95.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu ilibuni, kutekeleza na kushiriki kwenye miradi mbalimbali. Miradi hii ni pamoja na Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi, Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi, Mradi wa Kuboresha Mipaka ya Kimataifa, Mradi wa Kuwezesha Ushindani katika Sekta Binafsi (Sekta ya Ardhi), Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa

Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Bomba la Mafuta na Reli ya Kisasa.

***Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi***

**96.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imetekeleza Program hii yenye lengo la kuhakikisha milki salama kwa wananchi. Kiasi cha shilingi bilioni **10.8** zilitolewa na Serikali kutekeleza mradi huu. Kati ya hizo, shilingi bilioni **8.36** zilitolewa ili kuwezesha upangaji, upimaji, umilikishaji, ununuzi wa vifaa na ulipaji wa fidia katika Halmashauri **27** nchini. Jumla ya viwanja **37,351** vilipimwa na hatua za umilikishaji wake zinaendelea (**Jedwali Na. 19**). Vilevile jumla ya shilingi bilioni **2.44** zilitumika kuandaa mpango kabambe wa Jiji la Dodoma, kuandaa mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Morogoro na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila **5,845.** Vilevile vipande vya ardhi **134,239** vilitambuliwa na leseni za makazi **868** zilitolewa katika jiji la Dar es Salaam. Wizara itaendelea kuzijengea uwezo na kuziwezesha Halmashauri kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

***Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi***

**97.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imetekeleza Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi *(Land Tenure Support Programme)* katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi kuanzia Januari, 2016 kwa kushirikiana na mashirika ya maendeleo ya Serikali za Uingereza (DFID), Sweden (SIDA), na Denmark (DANIDA). Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imekamilisha utekelezaji wa Programu hiyo mwezi Disemba, 2019. Programu hii imewezesha uandaaji wa Mipango mitatu (**3**) ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Mipango hiyo imebainisha mgawanyo wa rasilimali mbalimbali katika kila Wilaya. Vilevile, jumla ya mipaka ya vijiji **129** imepimwa katika Wilaya za Kilombero (**65**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**22**). Pia, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **119** imetayarishwa katika Wilaya za Kilombero (**50**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**27**) (**Jedwali Na. 20**). Wataalam **32** wa Halmashauri hizo wamejengewa uwezo kuhusu uandaaji na usimamizi wa Mipango hiyo. Aidha, halmashauri hizo ziliwezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vya

upimaji na mafunzo ya matumizi yake.

**98.** ***Mheshimiwa Spika;*** Programu hii imewezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **182,126** kwa wananchi katika wilaya za Kilombero (**76,750**), Ulanga (**62,055**) na Malinyi (**43,321**). Hati hizo zimewawezesha wananchi kuzitumia kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo yenye thamani ya takriban shilingi bilioni **1.64** kutoka benki za CRDB, NMB na TADB. Sehemu kubwa ya wanufaika wa mikopo hiyo wameitumia mikopo yao kuwekeza katika shughuli za kilimo na biashara.

**99.** ***Mheshimiwa Spika;*** Programu hii pia imewezesha ujenzi wa ofisi za ardhi za Halmashauri za wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Vilevile, jumla ya vijiji **75** vimewezeshwa kukarabati masjala za ardhi za vijiji kwa ajili ya kutunza nakala za hati zilizoandaliwa. Wajumbe **641** wa Mabaraza ya Kata **66** na wajumbe **1,102** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji katika vijiji **129** wamejengewa uwezo kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya 2002 na Sheria

ya Ardhi Na. 4 ya 1999 zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa zaidi sheria na kanuni za sekta ya ardhi, ambapo nakala **15,000** zilichapishwa na kugawiwa kwa wananchi.

***Mradi wa Upimaji Mipaka ya Kimataifa***

**100.** ***Mheshimiwa Spika*;** katika kuimarisha usalama, maendeleo na ushirikiano barani Afrika, Umoja wa Afrika ulifikia makubaliano ya kuhakiki mipaka ya nchi za Afrika ili kutatua migogoro ya mipaka iliyowekwa enzi za ukoloni. Lengo la zoezi hili lilikuwa kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka kati ya nchi na hivyo kuepuka kutokea migogoro baina ya nchi. Azimio namba ***Assembly/AU/Dec.369 (XVII)*** lililofikiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika huko Durban na baadaye kufuatiwa na kikao kilichofanyika Malabo, Equatorial Guinea tarehe 30 Juni hadi 1 Julai, 2011 kilizitaka nchi zote za Afrika zihakiki mipaka yake na nchi jirani ifikapo mwaka 2017. Hata hivyo, muda huo uliongezwa tena hadi mwaka 2022 baada ya utekelezaji kutokamilika.

**101.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza azimio hilo, Wizara imeimarisha jumla ya **km. 369.9** za mpaka kati ya **km. 1,841** ya mipaka ya nchi kavu kati ya Tanzania na nchi jirani kama ifuatavyo: Tanzania na Kenya (**km. 172**), Tanzania na Msumbiji (**km.51**), Tanzania na Zambia (**km. 11.9**) na Tanzania na Burundi (**km. 135**). Aidha, Wizara inaendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu iliyobaki na mipaka ya ndani ya maji yenye jumla ya **km. 2,086** kabla ya mwaka 2022.

***Mradi wa Kuwezesha Ushindani wa Sekta Binafsi (Sekta ya Ardhi)***

**102.** ***Mheshimiwa Spika*;** mradi huu ulianza kutekelezwa chini ya uratibu wa ofisi ya Waziri Mkuu kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya biashara nchini. Kwa upande wa sekta ya ardhi, mradi ulilenga:- (i) Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kusanifu na kutengeneza mfumo unganishi wa kielektroniki wa taarifa za ardhi, (ii) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha taarifa za ardhi, (iii) Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji na uwekaji wa alama za msingi za upimaji. Kwa kipindi cha miaka mitano, mradi umewezesha kuundwa na kusimikwa kwa mfumo wa

ILMIS katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jumla ya kumbukumbu za majalada yenye taarifa **728,370** za usajili wa hati; upimaji na umilikishaji wa ardhi yamebadilishwa kutoka mfumo wa analojia na kuwa wa kidijitali. Viwanja **239,317** viliingizwa kwenye mfumo wa ILMIS na hatimiliki za ardhi **3,868** ziliandaliwa na kutolewa kwa njia ya kielektroniki. Aidha, jumla ya miamala **254,944** ilifanyika kupitia mfumo huo. Uanzishwaji wa mfumo wa ILMIS umehusisha pia ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu za Ardhi kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kitatumika kuhifadhi kumbukumbu zote za ardhi kwa njia ya kielektroniki kwa nchi nzima. Vilevile, mradi huu umewezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji vilivyosambazwa katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na uwekaji wa mtandao wa alama za msingi ardhini.

***Ushiriki wa Wizara katika Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa***

**103.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli za miradi ya Kitaifa ambayo ni Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, ujenzi wa Bomba

la Mafuta kutoka Hoima, nchini Uganda mpaka Chongoleani – Tanga pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa. Katika utekelezaji wa miradi hii ya Kitaifa Wizara imeshiriki katika upangaji, upimaji na uthamini wa mali katika maeneo ya miradi.

*Mradi wa uzalishaji umeme wa Julius Nyerere*

**104.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika uendelezaji wa eneo la mradi, Wizara inaendelea kuandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan) utakaowezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika ukanda huu. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 jumla ya mipangokina **19** yenye viwanja **4,309** iliandaliwa katika mji mdogo wa Kisaki na upimaji unaendelea. Aidha, mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji cha Mloka wenye matumizi ya Makazi, uwekezaji, hifadhi za wanyamapori, utalii, kilimo, misitu na vyanzo vya maji uliandaliwa. Katika mpango huo jumla ya viwanja **1,342** vimepangwa kwa ajili ya makazi (**1,110**), biashara (**217**), hoteli za kitalii (**15**) na matumizi mengine.

**105. *Mheshimiwa Spika;*** Shughuli nyingine zilizotekelezwa na Wizara yangu ni uwekaji alama za Upimaji ardhi nne (**4**) kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na upimaji wa hekta **1,402** za eneo la kujenga mitambo ya umeme kwenye maporomoko ya Mto Rufiji na hekta **4,711** kwa ajili ya ujenzi wa karakana na makazi ya mradi wa umeme. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kuratibu uandaaji wa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

*Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa*

**106. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaa rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan). Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Maeneo yote yaliyopendekezwa kuwa vituo vya treni na kwa matumizi mengine yanayohusiana na reli, yametambuliwa na taratibu za kisheria za kuyatangaza kuwa maeneo ya kimipangomiji zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea na

uandaaji wa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi, utangazaji wa maeneo ya miji midogo na uratibu wa uandaaji wa mipangokina na mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji.

*Mradi wa Ujenzi wa Bomba la mafuta*

**107. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaa pia, rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji ukanda wa mradi wa Bomba la Mafuta. Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Mamlaka za Upangaji za Wilaya za Misenyi, Bukombe, Kondoa, Handeni na Muheza zimeandaa Mipangokina katika maeneo yatakayojengwa kambi na mitambo ya mafuta. Mipangokina iliandaliwa kama ifuatavyo: Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi viwanja **306** vimepangwa na kupimwa katika eneo la Bulifani; Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe viwanja **341** katika eneo la Bukombe mjini; Halmashauri ya Kondoa viwanja **794** katika eneo la Serya; Halmashauri ya Muheza viwanja **185** katika eneo la Komoza na viwanja **144** katika eneo

la Kwedigongo pamoja na eneo lenye ukubwa wa ekari **44.93** katika eneo la Tanganyika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

### *Miradi mipya ya Wizara*

**108.** ***Mheshimiwa Spika;*** ili kuongeza usalama wa milki ya ardhi nchini na kuboresha makazi, Wizara imebuni miradi miwili (**2**) ambayo inatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/21. Miradi hiyo ni: -(i) Mradi wa Kuboresha Milki utakaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mradi huu una lengo la kusajili milki za ardhi milioni **2.5**, kuboresha Mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, Ujenzi wa Ofisi za ardhi za Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini na, kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya ardhi na taasisi zilizo chini ya Wizara. (ii) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani utakaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kupitia Benki ya Exim. Mradi huu una lengo la kuandaa ramani za msingi za upimaji, kuimarisha vituo vya upimaji katika miji mikuu yote na kuongeza alama za msingi za upimaji, kujenga kanzidata ya

taarifa za kijiografia pamoja na mifumo ya kulinda taarifa hizo kwa watumiaji na kujenga uwezo wa wataalam wa upimaji.

## 5.6 USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**109.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu pia inaratibu na kusimamia shughuli za taasisi mbalimbali. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

### Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**110.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kusimamia na kuratibu uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na utekelezaji wake katika maeneo ya vijiji na Wilaya, kutoa miongozo na elimu kwa umma na mamlaka za upangaji wa namna ya uandaaji wa mipango hiyo na matumizi ya ardhi. Mipango hii inasaidia kuainisha matumizi mbalimbali ya ardhi; kuwezesha ardhi kutumika kwa ufanisi na tija; kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi; na kutoa miongozo kwa mamlaka za upangaji katika kuandaa,

kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi.

**111.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kupitia Tume imeweza kuhuisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013–2033), kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya **7**, vijiji **692,** na mipangokina ya vitovu vya vijiji **17**, kushiriki katika miradi ya kimkakati ya kitaifa, na kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kupanga matumizi ya ardhi nchini (**Jedwali Na. 21**). Sambamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, migogoro ya mipaka katika vijiji **210** vinavyopakana na Hifadhi ya Serengeti pamoja na Hifadhi za Taifa za Misitu ilitatuliwa. Aidha, kwa kipindi hicho Tume imetoa mafunzo kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya **83** na watendaji wa Halmashauri za Vijiji **692** katika vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya Ardhi kote nchini.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***; vilevile Wizara yangu kupitia Tume kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau imeendelea kupanga, kupima na

kutoa Hati za Hakimiliki za kimila kwa wananchi katika vijiji mbalimbali nchini. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kupitia Tume imewezesha upimaji na uandaaji wa hati za hakimilki za kimila **21,790** katika vijiji **42** vilivyopo katika Wilaya za Kondoa, Mvomero, Uvinza, Urambo, Magu, Mkalama, Nzega, Kibondo, Korogwe, Muheza, Monduli, Babati, Bunda na Tarime. Wizara kupitia Tume itaendelea kuhakikisha kuwepo kwa milki salama za ardhi kwa wananchi.

**113.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kukamilisha mapitio ya Programu ya Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013–2033) ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Tume imekamilisha mapitio ya Programu hii. Kwa mwaka 2020/21, Wizara yangu kupitia Tume itaendelea kuhamasisha na kuratibu utekelezaji wa Mpango huo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia Tume iliahidi kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **95** kati ya **349**

katika maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA). Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara kupitia Tume imeweza kuratibu na kusimamia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji **94** vinavyopakana na Hifadhi za Taifa na Misitu ya Hifadhi. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara kupitia Tume itaendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na wadau pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo.

**115.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia Tume iliahidi kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **236** katika Wilaya na vijiji vinavyopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara kupitia Tume imewezesha kufanya uchambuzi wa maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 236 vinavyopitiwa na Bomba la Mafuta (EACOP). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Tume inatarajia kuwezesha upangaji matumizi ya ardhi ya vijiji **100** katika Wilaya zinazopitiwa na njia ya Bomba

la Mafuta (EACOP) na Wilaya zilizo mipakani mwa nchi.

**116.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu kupitia Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika kanda za maeneo ya kilimo pamoja na maeneo yanayopitiwa na miradi ya kimkakati. Maeneo hayo ni pamoja na maeneo inakotekelezwa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP) na maeneo yenye vyanzo vya maji ya mto Rufiji unakotekelezwa mradi wa uzalishaji wa umeme (*Mwalimu Nyerere Hydro Electric Dam Project*).

**Shirika la Nyumba la Taifa**

**117.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilitekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba nchini. Katika kipindi cha miaka mitano (2015/16 hadi 2019/20), Shirika lilitekeleza jumla ya miradi **99** ambapo kati ya hiyo, miradi **62** imekamilika. Kupitia miradi hiyo jumla ya nyumba **6,273** zilijengwa ambapo kati ya hizo, nyumba **1,617** ni za ofisi na

biashara, nyumba **3,036** ni za makazi na biashara na nyumba **1,459** ni za makazi. Kati ya nyumba za makazi, nyumba **1,185** zilijengwa kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini na nyumba **274** zilijengwa kwa ajili ya watu wa kipato cha kati (**Jedwali Na. 22**). Vilevile, Shirika linaendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji Miji ya Pembezoni *(Satellite Towns)* katika maeneo ambayo yanamilikiwa na Shirika ambayo ni Luguruni-Ubungo (**ekari 156.53**), Uvumba - Kigamboni (**ekari 202**) na Kawe- Kinondoni (**ekari 267.71**), Burka / Matevesi-Arusha Jiji (**ekari 579.2**) na eneo la Usa River - Meru (**ekari 296**).

*(NHC) lilipo eneo la Mutukula mkoani Kagera*

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha miaka mitano, Shirika limeuza nyumba za makazi **1,595** kwa wateja wapya katika miradi ya nyumba za makazi iliyoko katika maeneo mbalimbali nchini. Hii ni sehemu ya nyumba za makazi **2,879** za kuuza ambazo zinajumuisha nyumba zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa. Walengwa katika ujenzi huu ni wananchi pamoja na Halmashauri za wilaya. Kwa upande wa maeneo ya biashara na ofisi, Shirika limefanikiwa kuuza mita za mraba **2,144.70** katika miradi

mbalimbali yenye maeneo maalum ya ofisi na biashara yenye jumla ya mita za mraba **50,970** katika miradi ya *Morocco Square* na *Victoria Place*.

**119.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamia Dodoma, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa iliahidi kuanza ujenzi wa nyumba **1,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Shirika limefanya upembuzi yakinifu wa mradi huu na kuwasilisha taarifa yake Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata idhini ya kukopa kiasi cha takriban shilingi **bilioni 20** kutoka Mfuko wa Mradi wa Nyumba ili kuanza ujenzi wa nyumba hizi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Shirika lilikuwa katika hatua za mwisho za upatikanaji wa fedha hizo. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Shirika linatarajia kuanza ujenzi wa nyumba **400** kwa awamu ya kwanza.

**120.** ***Mheshimiwa Spika*****;** katika mwaka wa fedha 2019/20 Shirika linaendelea kusanifu, kusanifu na kujenga, kumalizia ujenzi, kukarabati au kusimamia ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma pamoja na

ofisi za taasisi mbalimbali za Serikali nchini ikijumuisha:-

(i) Ukarabati na upanuzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Jiji la Dodoma;

(ii) Ujenzi wa ukuta wa uzio wa Bodi ya Wahandisi Tanzania Jijini Dodoma;

(iii) Ujenzi wa majengo ya ofisi zilizoko Jijini Dodoma katika eneo la Mtumba za Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Ardhi; Wizara ya Viwanda na Biashara; na Wizara ya Nishati;

(iv) Ujenzi wa jengo la ofisi ya EWURA Medeli, Jijini Dodoma;

(v) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, Musoma;

(vi) Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa (Modern Abbatoir), Vingunguti, Dar es Salaam;

(vii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwl J.K. Nyerere iliyopo Kwangwa, Musoma, Mkoani Mara;

(viii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara;

(ix) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda, Mkoani Katavi;

(x) Ujenzi wa Majengo 44 ya Ofisi na Makazi kwa ajili ya Wakala wa Misitu Tanzania katika sehemu 17 mbalimbali nchini;

(xi) Ujenzi wa Shule ya Msingi ya watoto wenye mahitaji maalumu Mbuye, mkoani Geita; na

(xii) Usanifu na usimamizi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Fedha katika eneo la Mtumba, mkoani Dodoma.

**121.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika limegawanya utekelezaji katika mikakati ya muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu. Katika muda mfupi, Shirika limelenga kuboresha hali ya ukwasi (liquidity position) ili kuwa na fedha za kutosha kujiendesha. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kubana matumizi kwa kuondoa baadhi ya matumizi yasiyo ya lazima;

(ii) Kupunguza matumizi ya matengenezo ya nyumba bila kuathiri ubora wa nyumba;

(iii) Kutekeleza mpango wa kupanga upya baadhi ya mikopo yake (loans restructuring plan) ili kupunguza kiasi cha malipo ya mikopo kwa mwezi;

(iv) Kupangisha nyumba zote za gharama nafuu ambazo zilikuwa zimekamilika na bado hazijapata wanunuzi ili kuongeza kipato cha Shirika kutokana na kodi ya pango;

(v) Kukamilisha ujenzi wa baadhi ya miradi midogo na ya kati (ya nyumba za makazi na biashara) ambayo ilikuwa imesimama na kuipangisha na/au kuiuza ili kuongeza kipato cha Shirika; na

(vi) Kuchukuwa hatua mbalimbali za kukusanya madeni sugu ya wapangaji wa zamani na wa sasa na kuimarisha makusanyo ya kodi ya pango kwa wapangaji waliopo.

**122.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika muda wa kati, Shirika linalenga kumalizia miradi mikubwa ambayo imekwama na kuimarisha njia mbadala za mapato kwa Shirika ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Shirika. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutekelezaji miradi **26** ya ukandarasi na ushauri nchini kote yenye jumla ya thamani ya shilingi **bilioni 86.2**;

(ii) Kupitia upya mikataba ya wapangaji na kufanya maboresho ya vipengele ili kuhakikisha kwamba Shirika linakusanya kodi na madeni. Pia, wapangaji ambao wanakiuka masharti ya ulipaji wa kodi ya pango wanachukuliwa hatua za kisheria; na

(iii) Kufanya ukaguzi wa hali ya majengo yote ya Shirika (conditional assessment) ili kupanga mpango wa kuzifanyia maboresho na matengenezo ya kudumu nyumba zake ili kuziongeza thamani.

**123.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mikakati ya muda mrefu, Shirika linajipanga zaidi katika utekelezaji wa lengo lake kuu la kuwapatia wananchi makazi bora kwa kutanua wigo wa uwekezaji wake kama ifuatavyo:-

(i) Kubadilisha malengo ya nyumba mpya zitakazojengwa kutoka kuwa za kuuza **70%** na kupangisha **30%** na kuwa za kuuza **20%** na kupangisha **80%**; na

(ii) Shirika kuwekeza katika viwanda vya utengenezaji wa vifaa vya ujenzi kama vile kokoto, matofali na mabati.

**124.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika liliahidi kuandaa Mipango Kabambe ya Kwala (Ruvu) na mji mpya wa Kisarawe. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020, shirika linaendelea na hatua za awali za majadiliano na Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Kisarawe kuhusu mipango kazi ya upangaji wa maeneo ya pembezoni ya Kwala wilayani Kibaha na Vigungu Wilayani Kisarawe. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika litaendelea na utekelezaji wa mipango kabambe ya maeneo haya ya pembezoni ya Kwala na Vigungu.

**125.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika liliahidi kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi **bilioni 97**. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Shirika limekusanya jumla ya shilingi **bilioni 66** sawa na asilimia **69%** ya lengo. Aidha, shilingi **bilioni 2.9** zimekusanywa kutokana na mauzo ya nyumba na shilingi **bilioni 7.3** zikiwa ni mauzo ya viwanja. Katika

Mwaka wa Fedha 2020/21, Shirika limepanga kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi **bilioni 98.**

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi**

**126.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi inalo jukumu la kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na vifaa vya ujenzi wa nyumba. Katika kipindi cha miaka mitano, Wakala iliweza kufanya tafiti mbalimbali kuhusu vifaa vya ujenzi wa nyumba ikiwemo kununua mashine **200** za kufyatua vigae vya kuezekea nyumba na tofali.

**127.** ***Mheshimiwa Spika;*** mashine hizi zilizoundwa zimewezesha kufyatua vigae mkonge **170,000** na matofali ya kufungamana **100,000** yaliyouzwa kwa bei nafuu kwa wadau mbalimbali. Pia, Wakala katika kusambaza teknolojia ya mashine hizi iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya mashine kwa wananchi, vikundi na Taasisi za umma na binafsi katika mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Pwani, Manyara, Lindi, Mtwara, Geita, Kilimanjaro, Kagera, Tabora na Kigoma.

**128.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kuzingatia mabadiliko ya Muundo wa Wizara, Wakala umefutwa na majukumu yake yamehamishiwa Chuo Kikuu Ardhi kuanzia mwaka wa fedha 2020/21. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi na tija katika kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

**Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro**

**129.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inasimamia vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya fani mbalimbali za ardhi katika ngazi ya Astashahada (*Certificate*) na Stashahada (*Diploma*). Fani zinazotolewa ni upangaji wa miji na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani na sanaa, ubunifu na uchapishaji. Wizara imeendelea kuviimarisha vyuo hivi kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu, kuwezesha ujenzi wa majengo ya madarasa na ajira kwa wakufunzi wa elimu ili viweze kutoa ujuzi unaokidhi viwango vya taaluma zao.

**130.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Vyuo hivyo vinavyosimamiwa na Wizara vimeweza kudahili jumla ya wanafunzi **4,902**. Vilevile jumla ya wakufunzi watano (**5**) wa fani mbalimbali wameajiriwa katika vyuo hivyo. Katika kuimarisha utendaji kazi wa vyuo hivi, Wizara imeendelea kuwezesha ujenzi na ukarabati wa majengo **17** yenye vyumba vya madarasa **12,** mabweni **9** na maktaba **3**. Aidha, Mitaala ya kufundishia katika vyuo hivi imeendelea kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuiboresha. Wizara imeendelea pia kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kukipatia Chuo cha Ardhi Tabora vifaa na mitambo ya uchapishaji na kukifanya kuwa na uwezo wa kufanya machapisho ya nyaraka zote za wizara zinazotumika katika kazi za kila siku ikiwa ni pamoja na nyaraka za umilikishaji ardhi.

**131.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kuboresha miundombinu ya vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro ili kuviwezesha kuongeza udahili wa wanachuo. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Chuo cha Ardhi Morogoro kimeongeza udahili kufikia wanafunzi **427** kutoka

wanafunzi **274** waliodahiliwa mwaka 2018/19. Aidha, Chuo cha Ardhi Tabora kimeongeza udahili kufikia wanafunzi **1,271** mwaka 2019/20 kutoka wanafunzi **1,011** mwaka 2018/19.

**132.** ***Mheshimiwa Spika;*** ili kukidhi mahitaji ya fani mbalimbali za ardhi, vyuo vinakamilisha mapitio ya mitaala ya mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya astashahada na stashahada za upangaji wa miji na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro iliahidi kuandaa mwongozo wa Upangaji wa Makazi Vijijini utakaowezesha utoaji wa Mafunzo ya muda mfupi yatakayowajengea uwezo watendaji wa vijiji nchini. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara imekamilisha mwongozo huo na kuainisha aina za kozi mbalimbali zitakazofundishwa kwa watendaji wa vijiji nchini. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza mwongozo huu kwa mwaka wa fedha 2020/21. **Natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kushirikiana na vyuo**

**hivyo Kutoa Mafunzo kwa watendaji wote wa vijiji ili kuimarisha utawala wa ardhi katika maeneo ya vijiji.**

## 5.7 UTAWALA NA RASILIMALI WATU

**133.** ***Mheshimiwa Spika;*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Usimamizi huo unafuata sera, sheria na miongozo ya Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeweza (i) kuhuisha muundo wa Wizara ili kuendana na mahitaji halisi na mabadiliko ya sekta ya ardhi, (ii) kuhamisha watumishi wa sekta ya ardhi waliokuwa chini ya mamlaka ya OR-TAMISEMI kuwa chini ya mamlaka ya Wizara (iii) kuwapanga upya watumishi wa sekta ya ardhi katika halmashauri mbalimbali nchini kwa uwiano, (iv) kuanzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na kupeleka watumishi wa sekta ya ardhi ili kusogeza huduma za ardhi kwa wananchi, (v) Kusimamia nidhamu ya watumishi (vi) Upandishaji madaraja watumishi **442** kwa kuzingatia Miundo na Kada.

**134.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuwapanga upya watumishi wa sekta ya ardhi kwa uwiano. Katika kutekeleza azma hiyo na kwa kuzingatia agizo la Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuwahamishia watumishi wote wa sekta ya ardhi katika Wizara yangu, jumla ya watumishi **1,812** waliokuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wamehamishiwa katika Wizara na kupangwa upya kwa kuzingatia uwiano na mahitaji katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini.

***Utawala Bora na Uwajibikaji***

**135.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilipanga kuhuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa ufanisi sawia na maboresho ya mifumo yanayofanyika katika Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imeandaa rasimu ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Katika mwaka 2020/21, Wizara itakamilisha rasimu hiyo na kusambaza nakala katika Ofisi za Ardhi nchini na kwa wadau wa sekta ya ardhi. Pia Mkataba huo utawekwa

katika Tovuti ya Wizara.

**136.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kutekeleza mkakati wa kupambana na viashiria vya rushwa kwenye Sekta ya Ardhi kama sehemu ya mikakati ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa umma. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Mafunzo kuhusu maadili ya utumishi wa umma na mapambano dhidi ya rushwa yalitolewa kwa viongozi na watumishi pamoja na kula kiapo cha ahadi ya uadilifu. Aidha, watumishi **47** waliotuhumiwa kwa rushwa taarifa zao ziliwasilishwa kwa mamlaka husika kwa hatua.

**137.** ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kuajiri watumishi **56** kadri vibali vitakavyokuwa vinatolewa. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imeajiri jumla ya watumishi **42** wa kada mbalimbali kati ya hao, watumishi tisa **(9)** ni wa sekta ya ardhi na **33** wa kada saidizi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara imepanga kuajiri watumishi wa kada mbalimbali **270** kadri vibali vya ajira vitakavyokuwa vinatolewa ikiwa ni pamoja na

kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kustaafu.

***Mafunzo kwa Watumishi***

**138.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **304** kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020, Wizara yangu imewezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **154.** Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inaahidi kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **700** kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo ya watumishi wa Wizara na watumishi wa sekta ya ardhi waliohamishiwa Wizarani kutoka OR- TAMISEMI.

***Habari na Elimu kwa Umma***

**139.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kuendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Sekta ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Wizara iliandaa na kusambaza nakala **500** za kijarida cha Mwongozo wa Sheria za Mahakama za Ardhi, nakala **3,000** za vipeperushi (fliers) na nakala **1,500** za machapisho

mengine kuhusu shughuli za Sekta ya Ardhi. Aidha, vipindi **131** vya televisheni na redio kuhusu shughuli za Wizara viliandaliwa na kurushwa kupitia mitandao ya kijamii. Pia elimu ilitolewa kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo *facebook, instagram, youtube* na *twitter* na magazeti mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi.

## 6.0 SHUKRANI

**140.** ***Mheshimiwa Spika;*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuiongoza na kuisimamia Wizara hii na kwa maelekezo yake yaliyochochea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi chote cha Awamu hii. Kwa kipekee napenda kuwashukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yao yaliyoboresha utendaji wa Wizara

yangu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali tulioshirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa lengo la kuwahudumia watanzania. Nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa umahiri wenu katika kuongoza vikao vya Bunge. Napenda pia, kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango, maoni na ushauri wenu kwa kipindi chote cha Bunge hili.

**141.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kwa namna ya kipekee kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb.), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Bi. Mary Gasper Makondo, Naibu Katibu Mkuu Bw. Nicholas Mkapa, Dkt. Stephen Nindi Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Dkt. Maulid Banyani Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi kubwa

wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro pamoja na watumishi wote wa Wizara, kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kuhudumia umma wa Watanzania bila ubaguzi.

**142.** ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Upangaji, na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ikijumuisha Benki ya Dunia, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Mashirika ya Maendeleo ya DFID, SIDA na DANIDA. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**143.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda pia, kutoa shukrani kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa kwa kufanikisha upatikanaji wa Ofisi za Ardhi za Mikoa. Aidha, napenda kuzishukuru kampuni binafsi na Taasisi za Fedha zikiwemo *NMB, CRDB, NBC, Azania Bank, Stanbic Bank na TPB* kwa michango

yao. Pia nizishukuru taasisi binafsi na mamlaka mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kutekekeza majukumu ya Wizara ikiwemo Bodi za Kitaaluma za Wataalamu wa Mipangomiji, Wathamini na Wapima Ardhi na wamiliki wa kampuni za Upangaji na Upimaji. Vilevile, ninawashukuru wajumbe wa Kamati ya Ugawaji Ardhi, Baraza la Kitaifa la Ushauri wa Ardhi na Wenyeviti na Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## 7.0 HITIMISHO

**144.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuhitimisha kwa kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu imedhamiria kuendelea kufanya mageuzi kwa kutumia teknolojia za kisasa katika utoaji wa huduma za ardhi. Mageuzi hayo yanalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi na kijamii, kuimarisha usalama wa milki za ardhi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kuongezeka kwa pato la Taifa.

## 8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21

***Makadirio ya Mapato***

**145.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **bilioni 200** kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za Sekta ya Ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba hii.

***Makadirio ya Matumizi***

**146.** ***Mheshimiwa Spika;*** ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo: -

***Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi***

| AINA | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | **200,000,000,000** |
| | **AINA YA MATUMIZI** | **FEDHA** |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Matumizi ya Mishahara | 19,496,335,00 |
| | Matumizi Mengineyo | 27,482,305,00 |
| | **Jumla Ndogo** | **46,978,640,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 16,300,000,00 |
| | Fedha za Nje | 66,300,839,00 |
| | **Jumla Ndogo** | **82,600,839,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **129,579,479,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo shilingi **129,579,479,000/=**.

***Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi***

| AINA | AINA YA MATUMIZI | FEDHA |
|---|---|---|
| A | Matumizi ya Mishahara | 1,509,468,000 |
| B | Matumizi Mengineyo | 979,822,000 |
| C | Matumizi ya Maendeleo | 1,500,000,000 |
| | **Jumla** | **3,989,290,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi **3,989,290,000/=**.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili muweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **133,568,769,000/=**.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz.***

**149.** Mheshimiwa *Spika,* naomba kutoa hoja.